

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



21 JUNI, 2016



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA – 21 JUNI, 2016

### I. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU:

#### **399. MHESHIMIWA SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wafanyakazi wa migodi ya uchimbaji wa madini hufukuzwa kazi kiholela bila kulipwa fidia stahiki kutokana na ulemavu na magonjwa yanayosababishwa na vitendeakazi hatarishi wakati wakiwa kazini:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kuzuia kuingizwa nchini vitendea kazi hatarishi na kufunga migodi ambayo ina wahanga wengi wa ulemavu na magonjwa yatokanayo na shughuli za uchimbaji madini;
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza kutumia Sheria ya Fidia Namba 20 ya Mwaka 2008 ili wafanyakazi wa migodini walipwe fidia stahiki wanapopata ulemavu au ugonjwa wanapokuwa kazini, badala ya Sheria ya Fidia ya Mwaka 2002;

(c) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa waajiri wanaowatelekeza wafanyakazi waliopata ulemavu wakiwa kazini na kukataa kuendelea kulipa gharama za matibabu yao.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **400. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mji mdogo wa Mbalizi uliopo kwenye Halmashauri ya Mbeya ni kati ya Miji inayokua kwa kasi sana lakini inakosa miundombinu muhimu na uhaba wa maji pia:-

- (a) Je, ni lini Mji huo utapewa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji;
- (b) Je, ni lini Serikali itatatua tatizo kubwa la maji kwenye Mji huo;
- (c) Je, ni lini Serikali itajenga Vituo vya Afya kwenye Kata zilizo ndani ya Mji huo wa Mbalizi.

## **401. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Zahanati za Nyang'hanga, Salongwe, Nsola, Bundilya, Nyamahanga, Nyashigwe, Chabula, Ikengele, Isangijo, Langi na Lutale ziko kwenye hatua za ukamilishaji:-

Je, ni lini Serikali itazikamilisha Zahanati hizo.

## **402. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- (a) Je, Serikali itakubali kujenga Hospitali ya Wilaya ya Busokelo hasa ikizingatiwa kuwa Wananchi wametoa eneo tayari na wako tayari kushirikiana na Serikali;
- (b) Je, kama Serikali inakubali, ni lini kazi hiyo itaanza.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

### **403. MHESHIMIWA ALLY SALEH ALLY (MALINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Hivi karibuni Tanzania imetangaza kufungua ubalozi wetu nchini Israel ambapo Tanzania ilikata uhusiano hapo nyuma:-

- (a) Je, ni sababu gani zilizofanya kubadilika kwa mtazamo wa nchi na kurudisha uhusiano na Ubalizi;
- (b) Je, ni upi msimamo wa Tanzania katika suala la uhuru wa Palestina ambayo ndiyo iliyokuwa sababu kuu ya kukata uhusiano na Israel hapo nyuma.

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

### **404. MHESHIMIWA LUCY MICHAEL MLOWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Njombe – Makete kwa kiwango cha lami.

**405. MHESHIMIWA LOLESTIA JEREMIAH  
BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Gati la Bukondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**406. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI  
(MASWA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Bwawa la Maji la Kijiji cha Mwamihanza limejaa mchanga hivyo hukauka mapema hasa ifikapo nyakati za kiangazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulikarabati Bwawa hilo pamoja na miundombinu inayopeleka maji kwa Wananchi wa Kijiji cha Mwamihanza na Vijiji jirani.

## **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:**

### **407. MHESHIMIWA JUMA SELEMAN NKAMIA (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto:- Bei ya dawa za binadamu imekuwa ikipanda kila wakati na Serikali imekaa kimya wakati wananchi wake wanaumia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha chombo maalum cha kudhibiti bei ya dawa za binadamu hapa nchini.

### **408. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto:- Benki nyingi nchini zimekuwa na riba kubwa hali ambayo inafanya Wanawake washindwe kukopa ili kujiinua kiuchumi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Benki ya wanawake Mkoa wa Songwe ili wanawake wajasiriamali wanufaike na mikopo hii ya riba nafuu.

**DODOMA  
21 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**